

TANGAZO LA ZABUNI

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA

Simu. 028 280 4865
Nukshi 028 280 2719/2370
[Barua pepe: ded@kigomadc.go.tz](mailto:ded@kigomadc.go.tz)



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 332,
KIGOMA

12/02/ 2020

ZABUNI YA UPANGAJI JENGO/MAJENGO/ CHUMBA/ ENEO YA ZILIZOKUWA OFISI ZA HALMASHAURI YA WILA YA KIGOMA ZAMANI KABLA YA KUHAMIA KATA YA MAHEMBE.

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Shirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria vyenye nia na uwezo wa kupanga katika majengo 10 Kwa tangazo hili, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inapenda kuwaalika kutuma maombi ya kupanga kama yalivyo ainishwa hapo chini.

| S/N | JENGO | MCHANGANUO | NAMBA YA ZABUNI |
|-----|-------------------------------|--------------------|-------------------------|
| 1. | MAZINGIRA | Vyumba 2 | LGA/043/2019/2020/NC/1 |
| 2. | BIASHARA NA USHIRIKA | Vyumba 6 | LGA/043/2019/2020/NC/2 |
| 3. | KILIMO NA MIFUGO | Vyumba 9 | LGA/043/2019/2020/NC/3 |
| 4. | ELIMU NA UZIBITI UBORA | Vyumba 10 | LGA/043/2019/2020/NC/4 |
| 5. | ARDHI NA TSC | Vyumba 6 | LGA/043/2019/2020/NC/5 |
| 6. | AFYA | Vyumba 8 | LGA/043/2019/2020/NC/6 |
| 7. | MAENDELEO YA JAMII | Vyumba 12 | LGA/043/2019/2020/NC/7 |
| 8. | MANUNUZI | Vyumba 4 | LGA/043/2019/2020/NC/8 |
| 9. | YARD (KARAKANA) NA OFISI ZAKE | Yard na ofisi zake | LGA/043/2019/2020/NC/9 |
| 10. | OFISI ZA UVUVI | Vyumba vinne | LGA/043/2019/2020/NC/10 |

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani kamili ya mwombaji na namba ya simu inayopatikana muda wote.
2. Mwombaji aoneshe kiasi ambacho atalipa kwa kila mwezi kwa jengo, chumba au eneo analotaka kupanga. Aidha Mwombaji atatakiwa kueleza matumizi ya jengo, chumba au eneo analoomba.
3. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kupangishwa jengo/chumba/eneo zaidi ya moja kulinga na uwezo wake wa kifedha. Hata hivyo majengo

yanayoweza kupangishwa chumba kimoja kimoja ni katika majengo ya **Biashara na Ushirika** pamoja na jingo la **Kilimo na Mifugo**.

4. Mwombaji atatakiwa aambatishe kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai, cheti cha usajili wa namba ya mlipa kodi (TIN). Aidha mwombaji atakayeshinda atatakiwa kuwasilisha Hati ya uwakilishi ya Kisheria (Registered Power of Attorney). Pia kwa kampuni itakayoshinda itatakiwa kuwasilisha vielelezo halali vya kuonesha umiliki wa kampuni hiyo (memorandum na articles of association/ extract from the register).
5. Mwombaji aandike juu ya bahasha na kwenye barua ya maombi aina na namba ya zabuni aliyoomba. Atatakiwa kutuma kabrusha halisi (original) na nakala (copy) mbili (2) na ziwekwe kwenye bahasha moja. Juu ya bahasha kusindikwe wala kuwekwa alama yoyote zaidi ya jina la zabuni, namba ya zabuni na anuani ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kigoma.
6. Mtumishi au kiongozi wa ngazi ya kisiasa wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma hataruhusiwa kuomba zabuni.
7. Mwombaji ambaye sio raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atatakiwa kufuata taratibu za Kisheria za kiuwekezaji na biashara za nchi ya Tanzania.
8. Halmashauri ya Wilaya ya haitalazimika kuchagua zabuni yoyote ya kiwango cha juu au chini bali itazingatia vigezo vilivyowekwa na uamuzi wa bodi ya zabuni juu ya uteuzi ni wa mwisho.
9. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha ya kaki iliyofungwa ipasavyo (kwa Lakiri). Juu ya bahasha ionyeshwe aina ya zabuni, namba ya zabuni.
10. Waombaji wote wanashauriwa kufika maeneo ya majengo yalipo kabla ya kuomba ili kuweza kujiridhisha pamoja na kupata maelekezo itakapo bidi kutoka Ofisi ya zamani ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kuanzia saa 8.00 asubuhi mpaka saa 9.30 alasiri siku za kazi.
11. Maombi ya Zabuni zote yawasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Kigoma iliyopo Kata ya Mahembe eneo la Shule ya Msingi Mahembe. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe **17/02/2020 saa nne (10.00) kamili asubuhi siku ya Jumatatu**. Aidha waombaji au wawakilishi wote, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utafanyika tarehe **17/02/2020** saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Kigoma (Mahembe).
12. Maombi yote yatakayoletwa baada ya muda ulioainshwa kwenye kipengele cha 11 cha tangazo hili hayatapokelewa.

ALEX D NTIBONEKA

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA.**